

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA

ISO 9001:2015 CERTIFIED



**UJUMBE MAHSUSI KWA VITUO VYA
UTANGAZAJI VYA REDIO NA TELEVISHENI NA
WENYE LESENI ZA MAUDHUI MTANDAO**

Naomba kutumia fursa hii kufikisha ujumbe mahususi kwa vyombo vya Utangazaji vikijumuisha vituo vyote vilivyopewa leseni na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania kwa ajili ya kutoa matangazo kwa umma kwa lengo la kuelimisha, kuhabarisha na kuburudisha.

Vyombo hivyo ni pamoja na Redio na Televisheni zinazorusha matangazo kupitia miundombinu ya ardhi, matangazo yanayopitia waya (Cable) na yale ya maudhui mtandao.

TCRA kuanzia mwezi Julai, ilikutana na vituo vya Utangazaji kwa ajili ya kutoa elimu na kukumbushana umuhimu wa kazifahamu Kanuni ndogo za Utangazaji wa masuala ya Uchaguzi (CODE ON POLITICAL PARTY ELECTIONS BROADCAST 2015)

Elimu hii ililenga kuhakikisha kuwa Watangazaji na waandishi wote wana elimu sahihi ya Kanuni hizi na kwamba watatangaza habari zote za Uchaguzi kwa weledi mkubwa.

Inasikitisha kuona kuwa tayari ukiukwaji wa Kanuni hizi umeanza kujitokeza. Hii inadhihirisha kuwa, ama vituo vyetu havizingatii matumizi ya Kanuni hizi, au inapuuza matumizi ya Kanuni hizi.

Vilevile imejidhihirisha wazi kuwa vituo vingi vya Utangazaji vina leseni lakini hawasomi masharti ya leseni hizo na kuhakikisha uhai wa leseni zao.

Kanuni ya Leseni za Mawasiliano ya 39 (2) inavitaka vituo vya Utangazaji kutuma maombi ya kuhuisha leseni zao mwaka mmoja kabla muda wa leseni zao kuisha muda wake.

Hivyo basi natoa rai kwa vyombo vya Utangazaji vyote kuzingatia Kanuni ndogo za Utangazaji wa masuala ya Uchaguzi na zile za Tume ya Uchaguzi ili ziwawezeshe kutangaza masuala ya Uchaguzi kwa weledi mkubwa na hivyo kudumisha amani ya nchi.

Vile vile nitoe wito kwa watumiaji wote wa mitandao ikiwemo ile ya kijamii hususani Wasimamizi wa makundi (Administrators) mbali mbali ya mitandao hiyo na Wanachama wa Vyama vyote kuzingatia matakwa ya kisheria kuhusu masuala ya uchaguzi tunapohusisha mitandao ya Mawasiliano.

Imetolewa na:

MKURUGENZI MKUU
MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA
27.08.2020